KANISA LA MENNONITE TANZANIA (KMT)
Nyerere Designated District Hospital
(Nyerere Hospitali Teule ya Wilaya ya Serengeti)
P.O. Box 38, Mugumu, Serengeti, Tanzania
Tel. +255 (0)762 334 444, E-mail nyerereddh@yahoo.com

Working Smart for Quality Health Services in God's Name

17.04.2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Hospitali Teule ya Wilaya ya Serengeti (Nyerere DDH) kupitia Kibali cha ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye kumb. Na. FA.10/128/01/"L"/257 cha tarehe 09/02/2023 inatangaza nafasi za kazi nane (8) kama ifuatavyo:-

KADA NA SIFA ZINAZOHITAJIKA:

1. **Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II (ANO II) TGHS B – Nafasi 1**
   SIFA ZA MWOMBAJI
   Awe amehitimu na kufaulu kidato cha Nne na au Sita na mwenye stashahada (Diploma) ya Uuguzi ya muda usiopungua miaka miwili kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na awe amesajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

KAZI NA MAJUKUMU

i. Kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga.
ii. Kukusanya takwimu muhimu za Afya.
iii. Kuwaelekeza kazi Wauguzi walio chini yake
iv. Kuelimisha Wagonjwa na Jamii kuhusu Elimu ya Afya.
v. Kutoa huduma za Kinga na Uzazi.
vi. Kufanya kazi nyinginezo atakazopangiwa na Kiongozi Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na Elimu, uzoefu na ujuzi wake.

2. **Muuguzi Daraja II (EN) TGHS A - Nafasi 1.**
   SIFA ZA MWOMBAJI.
   Awe amehitimu na kufaulu Kidago cha Nne na au Sita Cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na awe amesajiliwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

KAZI NA MAJUKUMU

i. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika Jamii, Hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
ii. Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa Afya katika sehemu yake ya kazi.
iii. Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi.
iv. Kutoa ushauri nasaha
v. Kutoa huduma za Kinga na Uzazi wa Mpango
vi. Kutoa huduma za Uzazi na afya ya Mama na Mtoto
vii. Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
viii. Kufanya kazi nyinginezo atakazopangiwa na Kiongozi Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na Elimu, uzoefu na ujuzi wake.

3. **Msaidizi wa Afya Daraja II. (Medical Attendant) –TGHOS A Nafasi 6**

SIFA ZA MWOMBAJI.

Awe amehitimu na kufaulu kidato cha Nne na au kupata Mafunzo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali Cheti cha Uhudumu wa Afya ngazi ya Jamii, wenye Uzoefu wa kazi za uhudumu kwa muda usiopungua miaka minne katika mojawapo ya fani au sehemu zifuatazo:- Uuguzi, Maabara, Meno au Mionzi.

KAZI NA MAJUKUMU.

i. Kufanya Usafi wa vifaa vya kazi usafi wa wodi na Mazingira.
ii. Kusaidia Wagonjwa wenye ulemavu na wasiojiweza katika kwenda haja (kubwa na ndogo) na kuoga.
iii. Kusaidia kumlisha Mgonjwa asiyejiweza
iv. Kuchukua nguo za Mgonjwa kuzipeleka kufuliwa.
v. Kuchukua sampuli za Mgonjwa kwa ajili ya Vipimo vya Maabara na kufuatilia matokeo.
vi. Kutayarisha vifaa kwa ajili ya kusafisha na kufunga majeraha.
vii. Kufuatilia mahitaji ya dawa kwa Wagonjwa kutoka hifadhi ya Dawa.
viii. Kufanya kazi nyinginezo atakazopangiwa na Kiongozi Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na Elimu, uzoefu na ujuzi wake.

MASHARTI YA JUMLA:-

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45.
2. Katika barua ya Maombi, Mwombaji aambatanishe, Wasifu wake **(CV),** Nakala ya vyeti vya taaluma, Nakala za vyeti na Matokeo ya Kidato cha Nne na au cha Sita, Nakala ya cheti cha kuzaliwa, Nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) na Nakala za vyeti mbalimbali kuzingatia sifa za kazi husika.
3. Mwombaji aweke Picha moja 1 (*passport size)* na aandike Jina nyuma ya picha.
4. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili na yatumwe kwa Mganga Mfawidhi, Nyerere DDH S. L. P. 38, Mugumu Serengeti kwa njia ya Posta, kwa barua pepe:- nyerereddh@yahoo.com.
5. Tarehe ya mwisho kupokea maombi ni tarehe **30/04/2023** Saa 9:30 Alasiri,

Wenye sifa Stahiki ndio watakaoitwa kwenye Mahojiano.

UTAWALA NYERERE DDH

NYERERE DESIGNATED DISTRICT HOSPITAL
P.O. Box 38
MUGUMU-SERENGETI